**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**
**SHULE YA SEKONDARI MAKANYA**

S.L.P 114

SAME

TAREHE.......................

**MZAZI/MLEZI WA....................................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO-2024/2025 SHULE YA SEKONDARI MAKANYA ILIYOPO WILAYA YA SAME MKOANI KILIMANJARO**

**1.0** .ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (Form V) katika tahasusi ya **HGK/HKL** katika shule ya sekondari Makanya. Shule hii ipo wilaya ya Same katika kijiji cha Makanya kando kando mwa Barabara kuu itokayo Dar es salaam kuelekea Arusha. Umbali kutoka stend ya Makanya utakakoshukia mpaka shuleni ni kilomita 3.Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..........................................................

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

- Sketi mbili rangi pipi kifua (Benjamin aqua) lazima ifike chini ya magoti pia sketi iwe na rinda box
- Mashati(2) meupe mikono mirefu
- Sweta 1 rangi ni ya pipi kifua (Benjamin Aqua)
- Soksi nyeupe jozi 2
- Nguo za kazi 2 (SHAMBA DRESS) draft rangi ya blue
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi na chenye kufunika miguu vya Kamba (MODAL HAVIRUHUSIWI)
- Vifaa vya michezo track suit moja rangi ya kijani yenye mkanda mweupe pembeni na raba za michezo
- Jezi ya michezo rangi ya blue bahari

**NB: KWA MWANAFUNZI WA KIKE WA KIISLAM ANARUHUSIWA KUVAA HIJABU NYEUPE TU**

**2.2 MICHANGO YA SHULE**

a) **Michango inayo paswa kulipwa na kila mwanafunzi**.

| | |
|---|---|
| **i). Uendeshaji wa shule** | **Tshs 65,000/=** |
| **ii). Nembo ya shule** | **Tshs 5,000/=** |
| **iii).Kitambulisho** | **Tshs 5,000/=** |
| **iv) Tahadhari** | **Tshs 5,000/=** |

Tanbihi: Jumla ya michango ni Tsh. 80,000/= kwa mwaka. Fedha hizo zilipwe katika akaunti ya shule benki ya NMB 40501200098 jina la akaunti ni Makanya Secondary School. Hakikisha umeandika jina kamili la mwanafunzi na kidato chake kwenye Pay in Slip.

**b) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**

i. Ream ya karatasi 2 (A4) kwa mwaka.
ii. Vitabu vya masomo yaTahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
iii. Mashuka rangi ya pink 2, blanketi, mito 2 na foronya zake rangi ya pink
iv. Godoro (2½ x 6)
v. Chandarua 2½ x 6
vi. Vyombo vya chakula
vii. Ndoo mbili (lita 10)
viii. Jembe lenye mpini na hard broom kwa ajili ya usafi kwa wanafunzi wote.
ix. Madaftali makubwa ya kutosha (counter books quire 4)
x. Sanduku la bati(tranka)

**2.3. MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA**

a) Mwanafunzi aje na copy ya cheti cha kuzaliwa
b) Cheti cha kuhitimu kidato cha nne (leaving certificate)
c) Nakala ya cheti cha kidato cha nne (results slips)
d) Begi la kubebea madaftari na vitabu
e) Madaftari madogo kwa ajili ya mazoezi ya kila siku darasani
f) Picha passport zize nne ziwe zimepigwa na shati jeupe
g) kila mwanafunzi atajigharamia matibabu wakati wote awapo shuleni

**h)** mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu ya mkononi shuleni kabisa (kwa mawasiliano atembee na namba za simu zifuatazo:- mkuu wa shule 0713 903803 Makamu Mkuu wa shule 0757002278.

## 3.0. SHERIA ZA SHULE

3.1. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aiodha inazingatia miomgozo yote inayotolewa na wazara yenye dhamana na Elimu nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mabo ya msingi yafuatayo mara tu anapowasili shuleni:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi,wanafunzi wenzie na jamii kwa ujumla
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli (shughuli za kitaaluma na kazi za nje)
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (enening preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shuhle na nyingine utakazopoewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wake
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
h) Lugha chafu, matusi,ugomvi,fitina,kupiga/kupigana ni mwiko kabisa kwa mwanafunzi
i) Wizi wa aina yoyote ni mwiko kwa mwanafunzi
j) Unywaji wa vileo,kuuza pombe na uvutaji wa aina yoyote ni mwiko kabisa kwa mwanafunzi
k) Kuvaa sre za shule wakati wote unapokuwa shuleni(nguo zingine nje ya sare/maagizo ya shule haziruhusiwi)
l) Uharibifu na upotevu na mali binafsi na mali za umma ni kosa na utawajibika kulipa mali husika
m) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa akiwa bado mwanafunzi.Akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na uhusiano wa kimapenzi. Akibainika atafukuzwa shule.
n) Wageni wataruhusiwa kuwaona/kuonana na wanafunzi baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu kila jumapili ya mwisho wa mwezi tu.
o) Ni mwiko kwa mwanafunzi yoyote kwenda nyumba za walimu na wafanyakzi bila ruhusa ya pekee kutoka kwa mwalimu mlezi
p) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkinoni.
q) Mgomo wa aina yoyote ni marufuku na haramu
r) Mwanafunzi atapokea maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule
s) Mwanafunzi atajisafirisha mwenyewe wakati wa likizo au pale atakaporudishwa nyumbani/kufuzwa shule

### 3.2 Makosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi afukuzwe shule

i. Wizi
ii. Uasherati,ushoga,ubakaji,kuoa au kuolewa
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama cocaine,kubeli nk
iv. Uvutaji wa sigara

v. Kupiga au kupigana kwa mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yoyote na makosa mengine ya jinai
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Kudharau bendera ya Taifa
viii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako, walimu wa walezi na jamii kwa ujumla
ix. Kugoma kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
x. Kukataa kwa makusudi adhabu
xi. Kumiliki simu ya mkononi shuleni
xii. Kushiriki au kuendeleza imani za kishirikina
xiii. Kunyanyapaa au uonevu wa aina yoyote
xiv. Kuweka mimba ua kupata mimba
xv. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 60 bila taarifa/utoro
xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xvii. Kufanya jaribio la kujiua au kukatishia kama kunywa sumu n.k.

Karibu sana Makanya sekondari

..........................................

**BERNARD F. MGAYA**

**MKUU WA SHULE**

**FOMU NA 1 KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI**

**A: MWANAFUNZI**

1. JINA KAMILI……………………………………………………..
2. Shule ya " o" level uliyosoma…………………………………….
3. Namba ya mtihani………………………………………………….
4. Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………….
5. Nakubali nafasi niliyopewa/sitaki apewe mwingine(kata lisilihusika)
6. Nakiri/naahidi kutoshiriki migomo,fujo na makosa ya jinai
7. Sahihi …………………………………………………………….....

**B : AFISA MTENDAJI**

JINA……………………………………………………………………………………
KIJIJI/KATA…………………………………………………………………..WILAYA
……………………………………...MKOA………………………………………………..

Nathibitisha kuwa mwanafunzi…………………………………………………...ni mkazi wa kijiji/mtaa/kata hii na ni raia wa Tanzania

Sahihi…………………………………muhuri……………….tarehe……………………………

**C: MZAZI/MLEZI**

**JINA**……………………………………………………………………………………**.**
Nakubali mwanafunzi apate Elimu yake hapo Makanya Sekondari na kwamba atafuata sheria, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule na vinginevyo aadhibiwe. Pia atalelewa katika dini ya ………………………………………………………………

**FOMU NA 2. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

JINA LA MWANFUNZI...........................................................................................................
TAREHE YA KUZALIWA……………………………………………………………………..
JINSIA..........................................UMRI.......................................MAHALI UNAPOSIHI.......................................WILAYA.........................................MKOA.....................
SIMU NA.....................................................JINA LA BABA..........................................................................................YUPO HAI?.....................
JINA LA MAMA....................................................................................YUPO HAI?.....................

ANUANI.......................................................................................................................

SIMU NA.....................................................................................................................

KAZI YA MZAZI/MLEZI......................................................................................

**NB: TAARIFA ZA UONGO/ZISIZO SAHIHI ZITAPELEKEA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

**TUPATIE PICHA YA PASSPORT SIZE YA BABA MAMA /NA MLEZI WA KARIBU.**

## FOMU NA 3. MEDICAL EXAMINATIONS

**(To be completed by medical officer only)**

1. Pupil's name ……………………………………………………………………………
2. Age ………………………………………………………………………………….....
3. Blood count (white and red) ………………………………………………….............
4. Stool examination…………………………………………………..............................
5. Syphilis or/and other venereal diseases test……………………………………..........
6. T.B test…………………………………………………..............................................
7. Eye test…………………………………………………..............................................
8. Ears…………………………………………………...................................................
9. Abdomen…………………………………………………............................................
10. Spleen…………………………………………………..............................................
11. Urine for plamo test…………………………………….................................................

**12. ADDITONAL INFORMATION**

If any e.g physical defeats, impairment infections, pregnancy, chronic or family diseases etc

…………………………………………………..............................................

…………………………………………………..............................................

**I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION**

**STATION……………………………………………SIGNATURE……………………….**

**DATE……………………………………………DESIGNATION…………………...…**

**FOMU NA 4.**

**PLEASE IF POSSIBLE COME WITH THE FOLOWING BOOKS/REFERENCE/MATERIALS RELEVANT TO YOUR COMBINATION AS LISTED BELOW.**

1. **HISTORY**
   i. Major events in African Historyby Mwijage
   ii. The political economy and imperialism
   iii. Africa since 1800, 4th edition
   iv. The making of modern Africa
   v. How Europe under develop Africa
   vi. The 20th century by Duff M.N
   vii. Europe from 1815 by peacock
2. **Geography**
   i. Certificate of Geography (oxford) by mary Mugo Robert makugat and Paul kibuuka
   ii. General Geography in diagrams by R.B bunnet
   iii. Photography interpretation and elementary surveying for secondary A level
   iv. Regional Geography by Nyangwine and msabila
   v. Certificate human and economic Geography By Morgan and Leong Ghang
   vi. World Geographical Atlas
3. **English languages**
   i. English for A level practical approach 5&6
   ii. English language for A level 5&6
   iii. An enemy of the people
   iv. I will marry when I want
   v. The beautiful ones are not yet born
   vi. A man of the people
   vii. Divine providenve
   viii. His excellence the head of state
   ix. Betrayal in the sity
4. **General Studies**
   i. Understanding Advanced level general studies by J Bigirwamungu S S. Deogratius
   ii. General studies Notes (for A- level form V&Vi) by Mshiu and Nyangwine
5. **Kiswahili**
   **USHAIRI**
   i. Kimbung.G. Gorn (TUKI) 1994
   ii. Change Tamu.T.A Mvungi
   iii. Mapenzi Bora.M.S. Khatibu

**RIWAYA**

i. Vuta ni kuvute. Shafi A shafi
ii. Kufikirika na S. Robert
iii. Mfadhili na Hussein Tuwa
iv. Usiku utakapokwisha na mbunda msokile

**TAMTHILIA**

i. Morani na E Mbogo
ii. Kivuli kinaishi na Saidi Mohamed
iii. Kwenye ukingo wa Thim na E Hussein
iv. Nguzo mama (DUP) 1982.